## 102/3 – KISWAHILI KARATASI YA TATU - MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

1.

**(i) Sifa za malumbano ya Utani**

- Hufanywa na watu wawili au makundi mawili ya watu wanapokutana – kila utani una misingi na mipaka yake.
- Watu wenye uhusiano mzuri ndio hutaniana.
- Watani hufanyiana mizaha ambayo ina masharti yanayotawala uhusiano wao.
- Mbinu ya chuku hutumiwa kwa ubunifu mkubwa kusisitiza kejeli fulani / kutukuza tabia fulani.
- Huchukua njia ya ushindani, kila mmoja akijaribu kumpiku mwenzake.
- Wakati mwingine, watu hutania wale wasiokuwepo na aina hii ya utani huambatana na uigaji / uigizaji wa kuchelesha.

**(ii) Umuhimu wa Malumbano ya utani**

- Hupunguza urasmi miongoni mwa wanajamii – kujieleza kwa uwazi.
- Huimarisha urafiki / uhusiano mwema kwa wanaotaniana.
- Hutambulisha jamii kwa kutaja baadhi ya sifa zake katika utani.
- Hukosoa na kukashifu tabia hasi – baadhi ya Malumbao ya utani hudhihaki ulafi, uvivu, wivu n.k.
- Huburudisha – ucheshi katika malumbano ya utani huburudisha na kuchangamsha.
- Huelimisha – kupitia kwa malumbano ya utani, watu hupata maarifa ya kukabiliana na hali mbali mbali katika maisha.

b. Umuhimu wa:

**(i) Hodiya – nyimbo za kazi.**

- Huhimiza watu kutia bidii na kuendeleza kazi bila kufa moyo.
- Hukashifu uvivu na utegemezi.
- Hurahisisha kazi kwa kupunguza fikira za uchovu.
- Huonyesha changamoto zinazowakumba wafanyakazi na namna ya kukabiliana nazo.
- Kujenga ushirikiano wa watu wanaofanya kazi.

**(ii) Sifo:**

- Husifu matendo chanya ya viongozi au watu mashuhuri katika jamii.
- Hutangaza mafanikio / mchango wa mtu / watu wanaosifiwa kwa jamii.
- Hukuza uzalendo – kuiga matendo mema kutoka kwa wanaosifiwa.
- Huonyesha msimamo wa jamii kuhusu masuala fulani – wimbo unaosifu uzalendo kwa mtu fulani unaweza kuonyesha chuki kwa usaliti.
- Kuburudisha / hutumbuiza n.k.

**(iii) Bembelezi**

- Hutumbuiza na kuongoa watoto – hupumbaza na kumfanya mtoto alale au anyamaze anapolia.
- Hutumiwa kumsifu mtoto ambaye ni mtulivu, husifu mtoto na wazazi wake.
- Huonyesha mfumo wa kiuchumi wa jamii husika. Ikiwa baba ni msasi, mtoto atatajiwa kuwa baba ni msasi jasiri.
- Hukuza uhusiano wa mlezi na mtoto.
- Huelimisha mtoto kuhusu shughuli mbalimbali katika jamii.

**(iv) Mbolezi**

- Huonyesha msimamo wa jamii kuhusu kifo – Imani za jamii kuhusu kifo.
- Hutoa kumbukumbu na sifa za aliyekufa.
- Hufariji waliofiwa na kuwasaidia kukabiliana na uchungu / uzito wa aliyekufa.
- Ni njia ya kutakasa moyo na hisia za aliyefiwa.

2. (a) Mshairi anaeleza juhudi anazofanya mkulima akiwa kazini na matatizo anayopata katika kazi hiyo.
   - Ingawa mkulima anajitahidi licha ya matatizo yao, bado anahujumiwa haki yake na hafaidiki.
   - Ingawa mkulima ana bidii, amebaki kusononeka.

   (b) Inkisari (Kufupisha maneno)
   Mf. Yalomkabili – yaliyomkabili.
   Yendapo – yanapoenda.
   Hadhiye – hadhi yake.

   (c) (i) Kihisishi – kuonyesha jinsi mkulima alivyofanya kazi kwa mazingira magumu mno.
   (ii) Kiulizi – Mshairi anashangaa na kukasirishwa na hali ya kunyanyaswa kwa mkulima – unyanyasaji huu utakoma lin.
   (iii) Mtindo wa shairi
   - Tashbihi – kama jehanamu.
   - Balagha – kwa nini? Swali hili halihitaji jibu kwani wakulima wanaoulizwa hawapo kulijibu.
   - Takriri – hali ya kurudiarudia 'Nimeona.'
   - Taswira – Picha ya mkulima ambaye hana raha / jasho linamwagika.

   (d) Mshairi anaeleza kwamba ingawa mkulima anajitahidi katika kazi yake, hali yake haimariki na badala yake ni matatizo kuongezeka kwake.

**3) MSTAHIKI MEYA – TIMOTHY AREGE**.

(a) **<u>Tamaa</u>**.

(i) Dkt. Siki na Waridi wanataka sana kuhudumia wagonjwa (tamaa ya kazi yao.

(ii) Meya anapofika ofisini anadhihirisha tamaa kubwa ya maji hadi anamtuma Gedi amletee chupa moja.

(iii) Madiwani wana tama ya kubaki mamlakani ndiposa wengine wanafanya juu chini kuwa upande wa Meya.

(iv) Mstahiki Meya ana tamaa ya kusalia uongozini ndiyo maana anamhonga mhubiri awe upande wake na pia kutuma askari kukomesha wafanyakazi wanaogoma.

(v) Madiwani wengine wana tamaa ya kujinufaisha ndiyo sababu inakuwa vigumu kwake kuwa shawishi kujiunga naye kutetea wananchi.

(vi) Tamaa inadhihirika Meya anapomwarisha Diwani III kuwaongeza madiwani mishahara.

(vii) Visa vya ufisadi kama vile kunyakua mali ya umma vinasababishwa na tamaa.

(b) **<u>Uongozi mbaya</u>**.

(i) Meya anasema baraza lina malengo ya milenia kuona kuwa limepata maendeleo. Lakini hawafanyi chochote cha kuimarisha jiji. Siki anapobisha haya anaitwa mpambe na Gedi aamrisha kumtoa nje wa nguvu ilhali angeambiwa toke tu angetii.

(ii) Meya anakutana na baraza lake kujadili namna ya kukomesha mwamko wa umma. Wanakubaliana kutumia askari japo anawakumbusha wasiwe watu kuonyesha walikuwa wanaua. Anahofia kupoteza kura tu kwani ni mwaka wa uchaguzi.

(iii) Watu wanaletea chali zao za maisha ni mbaya ziimarishwe lakini madiwani nao wanaamua kutolipa kodi isitoshe wanapendekeza askari waongezwe msharaha na marupurupu mengine.

(v) Mstahiki Meya anasema atamfuta kazi mtu fulani bila kutoa sababu zozote ila tu kusema uongozi wake mpya unastahili kufanya kazi na watu wapya.

(vi) Anajitayarisha kuwapa wageni mapokezi ya kupigiwa mfano, atumie fedha nyingi badala ya kuboresha maisha ya wananchi wake walio na shida.

(vii) Meya anaamrisha idhaa ya baraza kucheza nyimbo za kizalendo, kabla na baada ya vipindi maarufu ili kupumbaza wananchi wadhani kila kitu kiko sawa.

(c) **Ubinafsi**.

(i) Viongozi wanalipora Baraza kujipa faida ya kibinafsi – mishahara ya madiwani iongezwe. Hashauriani na mtu.
(ii) Baraza linaahidi kuoa sadaka ya shilingi laki moja kila mwezi kwa mhubiri.
(iii) Hashauriani na yeyote.
(iv) Uk. 69 – Madiwani wana bima ya hospitali lakini watu wengine hawana wanalipia gharama ya matibabu.
(v) Meya ananyakua viwanja kadha vya ardhi ya Baraza yeye na wanandani wake.

(d) **Usaliti**.

(i) Viongozi hawa ni wa kuchaguliwa na wananchi. Kwa msingi ya kuwa watawasaidia katika kuimarisha hali yao ya maisha – kiuchumi, nafasi za ajira, kudumisha usalama, elimu na afya na kuleta uhusiano bora baina ya watu.

(e) **Kutowajibika.**

**Meya.**

(i) Anatumia mali ya baraza kiholelaholela (Kuuza fimbo ya meya).
(ii) Hajali hali ya hospitali (uwongo kuhusu madawa).
(iii) Hajali waslahi ya wafanyakazi (kutowalimizia madai yao)
(iv) Hajali elimu ya umma (kupeleka wanawe nje kwa elimu bora).
(v) Aamua mhubiri apate sadaka ya shilingi laki moja kila mwezi.
(vi) Apuuza ushauri bora na kuenzi mizengwe.
(vii) Atumia wahudumu wake (Gedi, Dida kama watumwa).
(viii) Atumia vyombo vya usalama vibaya.
(ix) Madiwani I na II hawamshauri Meya vizuri
(x) Wana tama ya faida ya kibinafsi.
(xi) Hawajali hali ya wafanyakazi na raia waliwachagua.
(xII) Hawajali hali ya hospiali.
(xiii) Wanakubali mali ya baraza itumiwe vibaya.

(f) **Ubadhirifu**

**Mifano**:

(i) Watoto wa Meya husomea nje ya nchi na hataki elimu ya kwao anayosema ni duni.
(ii) Apanga kuwapa mameya wageni dhifa ya kifahari ya kusimuliwa.
(iii) Anapanga kutumia pesa za Baraza kumfurahisha na kumvutia mhubiri.
(iv) Ananyakua viwanja vya baraza pamoja na wandani wake na kuuza kipata pesa kibinafsi.
(vi) Madiwani wanapoomba marupurup anakubali na kusema kuwa naye Bili apewe kama kwamba ni mshauri wa Baraza.
(vi) Afurahisha madiwani kwa kuongea mshahara wao kiholela.
Mifano zaidi
Propaganda Matatizo 10 x 2 = 20)

4) (a) **Haya ni maneno ya Meya**.

(i) Anawanenea Diwani I, II na Bili.
(ii) Wako ofisini mwake.
(iii) Wanapanga namna ya kuuza fimbo ili wajipatie pesa zaidi. (alama 4)

(b) (i) Njama ya kuiuza fimbo ya Meya. (alama 2)

(c) (i) Ufisadi
(ii) Wizi
(iii) Tamaa (2 x 1 = 2)

(d) (i) kunyanganya ndimi – grand idea. (1 x 2 = 2)

(e) (i) Katili
(ii) Mfisadi
(iii) Mbinafsi (3 x 2 = 6 ) 1 Kutaja, 1 Kueleza = 2

(f) (i) Mshahara duni
(ii) Ukosefu wa dawa hospitalini.
(iii) Umaskini
(iv) Vifo.
(v) Elimu duni. (4 x 1 = 4)

**4) RIWAYA : KIDAGAA KIMEMWOZEA**

i. Jinsi anwani inavyoafiki yaliyomo kitabuni
ii. Kitendo cha madhubuti cha kumpinga babake (Mtemi nasaba Bora) na kuanza harakati za kumng’oa mamlakani
iii. Uasi wa madhubuti kukataa kutafutiwa kazi kwa njia ya hongo na babake
iv. Gadaffi na wenzake kutaka kumuua Mtemi njiani
v. Lowela bintiye maozi kumwandikia Mtemi barua akimpa masharti makali
vi. Mwalimu majisifu kugunduliwa chuoni mkokotoni kuwa hakuwa mmiliki wa riwaya ya kidagaa kimemwozea
vii. Mwalimu majisifu kushindwa kuitolea mihadhara na kujibu maswali ya kidagaa kimemwozea.
viii. Mashaka kupata na wazimu baada ya Ben Bella kuamua kuvunja mapenzi kati yao.
ix. Amani kuamrisha Mtemi kumpa hati miliki zote za mali yake
x. Amani kupatikana katika chumba cha Mtemi usiku
xi. Amani kusukumiwa mzingo wa kukilea kitoto kisicho chake-uhuru
xii. Mwalimu majisifu na mkewe Dora kujaliwa watoto wote walemavu
xiii. DJ bob kung’atwa na jibwa Jimmy katika maskani ya Mtemi
xiv. Majununi kukataliwa na Michelle hata baada ya kujaribu kutimiza matakwa yake.
xv. Chweche mackweche kudumishwa baada ya kuvunjika paja lake hata baada ya kuiletea nchi fahari katika mchezo wa kandanda
xvi. Mzee matuko weye kudunshwa baada ya kupigania nchi yake katika vita vya Dunia.

6) **BARUA**

- Barua ya MacArthur Kuto (mkuu wa idara) kwa mwalimu majisifu kumwalika kwenda kutoa mhadhara katika chuo kikuu.
- Barua ya Ben Bella kwa mpenziwe Mashaka kumjulisha sababu za kuamua kumwacha kwake.
- Barua ya Madhubuti kwa babake ya kuonyesha uasi wake dhidi ya vitendo viovu vya babake.
- Barua ya Lowela maozi kwa mpenziwe mtemi akimtaka aachilie huru Amani na Imani.
- Barua ndefu tunayoelezwa vile mtemi Nasaba Bora ambayo aliandika akimwondolea lawama Yusufu . Barua hiyo ilikabidhiwa Amani na mwalimu Majisifu kama ushahidi.